



April 2016

Rafiki wapendwa,

Mwezi huu wa pili, Mungu amenialika kujiunga na nyinyi na kuwashirikisha matumaini ya kushangaza ya Yesu Kristo kwa wanawake kupidia Project Hannah. Kama mkurugenzi mpya wa kimataifa wa huduma, ninahamasika kupokea wajibu huu wa kulinda na kuongoza Project Hannah kwa siku zijazo. Nikiwa na shukrani kwako wewe, Marli Spieker, na kwa mamia ya wafanyakazi na watu wanaojitolea ulimwenguni, nasherehekea msingi imara uliouweka ambao tunajenga juu yake sasa.

Nataka tuanze safari yetu kwa kusema “asante sana” kwa maombi yako ya miaka mingi ukiwa na Project Hannah na kwa kutumia kalenda za maombi kama mwongozo. Wewe ni sehemu ya nguvu ya maombi kwenye nchi 125. Kwa pamoja, tunayaweka maombi yetu katika vitendo kupidia lugha 69 za huduma ya redio na kwa kuwafikia wanajamii na tunawasiliana kwa uaminifu kuhusu mahitaji ya wanawake ulimwenguni. Mungu anatenda kazi kubwa sana, na nina hamu ya kuona kile alicho nacho kwa ajili yetu kwa siku zijazo.

Mwezi huu tunawainua dada zetu wa Karibeani. Tuombe ili mioyo yao iguswe na maisha yao yaponywe katika Jina la Yesu. Waweze kuupata uzuri wake ndani mwao kama wanavyoona na kuufurahia uzuri wake unaowazunguka kwa namna ya uumbaji wake.

Maombi yako ya msisistizo yanatuunganisha kwenye msingi unaoimarisha kila hatua tuliyo nayo njiani. Bila maombi yako tusingeweza kufanikisha kazi aliyoiweka mbele zetu. Tunapoendelea kuomba, mioyo yetu inashangilia kwamba anayasikia maombi yetu. Yeye huchagua waliovunjika mioyo. Anatusamehe tunapotubu. Anatupa matumaini na uponyaji wa milele kupidia kwa mwanawewe Yesu (Zaburi 32:21; Zaburi 34:17; 1 Yohana 1:9; Yohana 3:16 na 15:5).

Nina shukurani za milele kwako wewe kwa kujitoa kwako kuwaombea wanawake ulimwenguni kote. Najua kuwa Mungu anawaona wanawake wetu na kusikia vilio vyao. Na tuendelee kusimama kwenye zamu kwa ajili ya dada zetu tunapoyaleta matumaini kwa wanawake ulimwenguni kote ili waweze kuwa kama Yesu.

Katika yeye mioyo yetu inashangilia,

Peggy Banks
Mkurugenzi wa Kimataifa wa Huduma
Project Hannah